# Dagaa dili soko la kimataifa

Na John Nditi, Morogoro

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imesema mazao ya uvuvi ikiwamo dagaa mchele na dagaa wa Kigoma yanahitajika kwa wingi katika soko la nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) pamoja na Marekani, Australia na Canada.

Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi, Emmanuel Bulayi alisema hayo juzi mjini Morogoro alipokuwa akifungua kikao kazi cha wanachama wa Jukwaa la Wanawake Wanaojihusisha na Shughuli za Uvuvi Tanzania (Tawfa).

Alisema kutokana na mahitaji makubwa ya mazao ya uvuvi hasa dagaa mchele wanaovuliwa Ziwa Victoria na Bahari ya Hindi kwenye masoko hayo, uzalishaji wake hususani dagaa mchele litakuwa ni suala la kimkakati la wizara na idara hiyo.

Alisema soko la ndani la mazao ya uvuvi bado ni kubwa hasa dagaa mchele na pia katika soko la kikanda kwenye nchi ya Zambia, Zimbabwe na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) ambako mahitaji yake ni makubwa.

Bulayi alisema licha ya masoko hayo, pia yapo masoko mengine na kutolea mfano wa dagaa wa Kigoma ambao wanahitajika na kusafirishwa soko la Marekani, Australia na Canada na kwamba wana bei nzuri na soko lake Tanzania haiwezi kutosheleza.

"Kwenye suala la masoko ya mazao ya uvuvi hatuna matatizo, tatizo lipo kwenye kupata taarifa na hizo taratibu za kimasoko," alisema Bulayi.

Alisema kutokana na mahitaji hayo makubwa, uzalishaji wa dagaa mchele utakuwa ni suala la kimkakati kwa wizara na idara hiyo kwa vile ndilo zao muhimu la uvuvi ambalo wanawake wengi wanashiriki.

Bulayi alisema pamoja na mkakati huo, kwa sasa asilimia 40 ya wanawake hapa nchini kwenye mnyororo wa shughuli za uvuvi ni wafanyabiashara na wachakataji.

Naye Mwenyeki Taifa wa Tawfa, Beatrice Mmbaga alisema baadhi ya sheria zimekuwa zikimbana mwanamke, hivyo kupitia jukwaa hilo changamoto nyingi zitatatuliwa na kuwafanya wanawake washiriki kikamilifu kukuza uchumi wa nchi na lishe bora kwa jamii.

Mratibu wa Shughuli za Mazingira katika Ukanda wa Pwani na Bahari ya Hindi kutoka Shirika la Mazingira Duniani (WWF) Ofisi ya Tanzania, Dk Modesta Medard alisema jukwaa hilo litawawezesha wanawake kufanya kazi pamoja, kujifunza na kuwezeshwa kwenye mnyororo wa thamani ya mazao ya uvuvi likiwamo zao la mwani kwenye Ukanda wa Pwani.



# Amref yatenga mil 200/ vikundi kilimo cha chai, kahawa

Na Frank Leonard, Iringa

SHIRIKA la kimataifa la Amref Health Africa limetenga zaidi ya Sh milioni 200 kuviwezesha vikundi vinavyojishughulisha na kilimo cha chai na kahawa katika wilaya za Kilolo na Mufindi, mkoani Iringa.

Mpango huo unatekelezwa kupitia mradi wa mwaka mmoja wa Usafi wa Mazingira na Uwezeshaji Wanawake (Wawe) ulioanza kutekelezwa na shirika hilo katika wilaya hizo hivi karibuni.

Mradi huo pamoja na lishe endelevu na usafi wa vyoo na maji salama kwa jamii inayojishughulisha na kilimo cha chai na kahawa.

Alisema kupitia mradi huo, vikundi vya ujasiriamali vya vijana na wanawake vitaanzishwa na kuhamasisha upatikanaji wa maji salama, vyoo bora na usafi wa mazingira kwa jamii hiyo.

"Kupitia ruzuku hiyo ya zaidi ya Sh milioni 200 tunatarajia vikundi hivyo vitaboresha vipato vyao vitakavyowawezesha kupata mlo na lishe bora, uzalishaji mali ulioimarika na kutumia maji salama na yenye uhakika katika kuchochea afya bora,"

Scanned with CamScanner